

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**BUNGE LA TANZANIA**

Simu: +255 026 2322761-5  
Fax No. +255 026 2324218  
E-mail: [cna@bunge.go.tz](mailto:cna@bunge.go.tz)



Ofisi ya Bunge,  
Mtaa wa Makole  
S.L.P. 941,  
**41105 DODOMA.**

**TAARIFA KUHSU VIKAO VYA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE**

Kamati nne (4) za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana tarehe 10 hadi 30 Oktoba, 2022 Jijini Dodoma. Kamati hizo ni Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI.

Kamati nyingine za Kudumu za Bunge zitaanza kukutana tarehe 17 hadi 28 Oktoba, 2022 Jijini Dodoma. Kamati zinaanza kukutana kabla ya Mkutano wa Tisa wa Bunge unaotarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 1 Novemba, 2022.

Shughuli zilizopangwa na Kamati za Bunge zinajumuisha maandalizi ya shughuli za Mkutano wa Tisa wa Bunge ambazo zinahusu Miswada minne ya Sheria na Taarifa za Kamati zinazosimamia Matumizi ya Fedha za Umma na Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ambazo ni PAC, LAAC na PIC. Shughuli zingine za Kamati ni kama ifuatavyo: -

- (a) Kamati ya Sheria Ndogo itafanya Uchambuzi wa Sheria Ndogo zilizowekwa mezani Bungeni wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge. Lengo ni kutekeleza masharti ya Kifungu cha 11 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;
- (b) Kamati Tisa (9) za Kisekta zitapokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji kwa mujibu wa Kifungu cha 7 (c) na (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020;
- (c) Kamati mbili (2) zinazosimamia matumizi ya fedha za umma zitachambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021. Lengo ni kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kuzingatia masharti ya Kifungu cha 14, Kifungu cha 15 na Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;
- (d) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) imepanga kupokea na kuchambua taarifa za uwekezaji wa mitaji ya umma. Lengo ni kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na miongozo mujarabu ya biashara. Shughuli hiyo imepangwa kama inavyoelekezwa na Kifungu cha 12 (1) na (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;

- (e) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama itapokea na kujadili Taarifa za Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki na za Wawakilishi wa Bunge la Tanzania katika Vyama vinne (4) vya Kibunge. Lengo ni kuzingatia masharti ya Kifungu cha 7 (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020;
- (f) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imepanga Kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama inavyoelekeza Kanuni ya 113 (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge; na
- (g) Kamati ya Masuala ya UKIMWI imepanga Kujadili Taarifa zinazohusu Afua za UKIMWI na Udhhibiti wa Dawa za Kulevya, kwa kufuata masharti ya Kifungu cha 10 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Shughuli hizo, pamoja na mambo mengine, zinatarajiwa kuwezesha Kamati nane kuandaa Taarifa zitakazowasilishwa Bungeni wakati wa vikao vya Mkutano wa Tisa wa Bunge. Taarifa hizo zitahusu: -

- (a) Uchambuzi wa Taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Hesabu za Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2021;
- (b) Uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji wa mitaji ya umma uliolenga kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na miongozo mujarabu ya biashara
- (c) Maoni kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa mwaka wa fedha 2023/2024.
- (d) Maoni kuhusu Miswada minne ya Sheria iliyosomwa mara ya kwanza wakati wa Mkutano wa Nane wa Bunge ambayo itajadiliwa wakati wa vikao vya Mkutano wa Tisa wa Bunge.

Ratiba za Shughuli za Kamati zote inapatikana katika Tovuti ya Bunge ambayo ni [www.bunge.go.tz](http://www.bunge.go.tz)

**Imetolewa na:-** Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,  
Ofisi ya Bunge,  
**DODOMA.**

**07 Oktoba, 2022**